

MKATABA WA UPANGAJI

MKATABA huu umetayarishwa leo tarehe 12 mwezi 05 mwaka 2022

KATI YA

..... wa Dar es salaam Tanzania (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama "MWENYE NYUMBA") kwa upande mmoja.

NA

LITTLE EGRET INVESTMENT COMPANY LIMITED wa S.L.P 7224 Dar es salaam (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama "MPANGAJI" kwa upande mwingine.

NA KWA VILE Mwenye NYUMBA amekubali kupangisha na Mpangaji amekubali kupangishwa sehemu ya nyumba (Chumba) hiyo kwa miaka SITA miezi 72 iliyopo Temeke kata ya Chan'gombe, Mtaa wa Temeke, Barabara ya Mandela, Namba ya kiwanja 123 Namba ya nyumba 123. namba ya kitalu D
HIVYO BASI Makubaliano hayo yameshuhudia yafuatayo

1. MUDA WA MKATABA

Mkataba huu utakuwa wa kipindi cha miezi 72 kuanzia tarehe 12 Mwezi 05 mwaka 2022 na utamalizika tarehe 12 mwezi 05 mwaka 2028

2. KODI

Mwenye nyumba amekubali kupangisha na mpangaji amekubali kupangishwa katika sehemu hiyo ya nyumba kwa madhumuni ya kufanya biashara/ofisi kwa kulipa kodi ya shilingi (500,000) kwa mwezi mmoja. Wakati wa kutiliana saina mwenye nyumba amekubali kupokea Tsh 6,000,000 ikiwa ni malipo ya miezi KUMI NA MBILI TU.

3. NI WAJIBU WA MPANGAJI KUTEKELEZA YAFUATAYO:-

- Kutopangisha Mtu mwingine katika nyumba hiyo bila idhini ya Maandishi ya Mwenye nyumba
- Kulipia gharama zote za umeme katika chumba hicho kwa kipindi cha Mkataba.
- Biashara ya kamali, kilevi na vitu vya haramu vyote havitakiwi 'na kama kuna ukarabati mkubwa haurusiwi kufanya mpaka uwasiliane na mwenye nyumba.
- Matengenezo madogomadogo anafanya mwenyewe pamoja na marekebisho yote madogo y kuboresha.
- Mpangaji anatakiwa kutoa taarifa mienzi miwili (2) kabla ya mkataba kumalizika kama anaendelea au haendelei.
NB; kuvunja moja ya masharti haya utakuwa umevunja mkataba.

4. NI WAJIBU MWENYE NYUMBA KUTEKELEZA YAFUATAYO:-

- Kuweka nyumba katika hali nzuri
- Kutombughudhi Mpangaji wa chumba hicho anayesimamia kwa masharti yaliyopo.

5. INAKUBALIWA PIA KUWA

- (a) Endapo Mpangaji atakuwa na Nia ya kuendeleza atawajibika kutoa taarifa ya Maandishi mwezi mmoja kabla ya kipindi cha Mkataba kuisha.
- (b) Kama Mpangaji hatakabidhi nyumba hiyo kama walivyokubaliana basi Mwenye nyumba an haki ya kumtoa kwa kutumia Dalali yeyote bila amri yoyote ya Mahakama.
- (c) Mgogoro wowote utatokea kuhusiana na Mkataba huu, basi mgogoro huo utatambuliwa kufuatana na sheria za nchi.

Mkataba huu umeshuhudiwa na wahusika kwa kutia sahihi zao katika namna na katika tarehe, mwezi na mwaka unaoonekana hapa chini.

UMESAINIWA na KUTOLEWA na
.....SALOME SANDRA..... ambaye amekubaliwa
Na ambaye namfahamu hapa Dar es salaam
Leo ⁰⁹ mwezi ⁰⁵ mwaka 2022.

[Signature]
.....
MWENYE NYUMBA

UMESAINIWA na KUTOLEWA
Na **LITTLE EGRET INVESTMENT COMPANY LIMITED**
ambaye amekubaliwa
Na ambaye namfahamu hapa Dar es salaam
Leo ⁰⁹ mwezi ⁰⁵ mwaka 2022.

[Signature]
.....
MPANGAJI


SHAHIDI;

JINA.....DANIEL SIMON.....

SAHIHI.....[Signature].....

ANWANL.....105069 DSM......

KAZI.....WAKILI......



STAMP DUTY
Tshs 60,000/= Collected
Receipt No. 99816659657 Date 17/05/2022
[Signature]
Regional Manager - Ilala Tax Region

W.H.TAP 600000/=
SD: 60,000/=
660,000/=
[Signature] 17/05/2022